


UTABIRI WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2026 – APRILI, 2027)



Kielelezo 1. Mwelekeo wa Mvua za Msimu (Novemba, 2026 hadi Aprili, 2027).

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

Dondoo muhimu za mvua za *Msimu* (Novemba, 2026 – Aprili, 2027)

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa mvua za Msimu kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (kanda ya magharibi, kati, nyanda za juu kusini magharibi, kusini mwa nchi, ukanda wa pwani ya kusini pamoja na maeneo yaliyopo kusini mwa Mkoa wa Morogoro) katika kipindi cha miezi ya Novemba, 2026 hadi Aprili, 2027. Ushauri na tahadhari umetolewa kwa wadau wa sekta mbalimbali wanaotumia taarifa za hali ya hewa katika utekelezaji wa majukumu yao kama vile kilimo na usalama wa chakula, mifugo na uvuvi, maliasili, wanyamapori na utalii, nishati na maji, ujenzi, usafiri na usafirishaji (nchi kavu, kwenye maji na angani), mamlaka za miji, afya, sekta binafsi pamoja na menejimenti za maafa. Muhtasari wa mwelekeo wa mvua hizo na athari zake ni kama ifuatavyo:

a) Mwelekeo wa mvua za Msimu kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka:

- i. Mvua za Msimu 2026/2027 zinatarajiwa kuathiriwa kwa kiwango kikubwa na hali ya El Niño yenye Nguvu Kubwa, hususan nusu ya kwanza ya msimu (Novemba 2026 hadi Januari 2027).
- ii. Mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Singida, Dodoma, Njombe, Iringa, Mbeya, Songwe, Rukwa pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro. Hata hivyo, mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi.
- iii. Mvua za Msimu zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Oktoba katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Tabora, Katavi, Kigoma, Lindi na Mtwara na kusambaa katika maeneo mengine mwezi Novemba 2026. Mvua hizi zinatarajiwa kuisha kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2027 katika maeneo mengi.
- iv. Mvua nyingi zinatarajiwa katika kipindi cha nusu ya kwanza ya msimu (Novemba, 2026 – Januari, 2027), ikilinganishwa na nusu ya pili (Februari – Aprili, 2027).

Athari na ushauri

- i. Vipindi vya unyevu kwenye udongo wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa mazao na miundombinu ya kilimo.
- ii. Ongezeko la kina cha maji katika mabwawa na mito linatarajiwa kujitokeza, hali ambayo inaweza kuathiri miundombinu ya rasilimali za maji na nishati.
- iii. Magonjwa ya mlipuko yanaweza kujitokeza kutokana na uchafuzi wa maji.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe: met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

1. MWENENDO WA MVUA ZA VULI, 2026 NA MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2026 HADI APRILI, 2027)

1.1 Mwenendo wa Mvua za Vuli (Oktoba-Desemba), 2026

Msimu wa Vuli, 2026 katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia) pamoja na Zanzibar (visiwa vya Unguja na Pemba)) utabiri wake ulitolewa tarehe 18 Agosti, 2026. Mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani zilitarajiwa katika maeneo mengi ya pwani ya kaskazini, nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa Ziwa Victoria.

Mvua hizo zimeshaanza katika maeneo machache ya ukanda wa Ziwa Victoria na pwani ya kaskazini kama ilivyotabiriwa. Ongezeko la mvua linatarajiwa katika miezi ya Novemba na Desemba, 2026. Aidha, mvua za nje ya msimu zinatarajiwa kuendelea katika mwezi Januari, 2027.

1.2 Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2026 hadi Aprili, 2027)

Mvua za Msimu ni mahususi katika maeneo ya magharibi mwa nchi, kanda ya kati, nyanda za juu kusini magharibi, kusini mwa nchi, ukanda wa pwani ya kusini pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro. Maeneo haya yanapata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, unaoanza mwezi Novemba na kuisha kati ya mwezi Aprili na Mei ya mwaka unaofuata.

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa (kama inavyoelezwa katika kipengele cha 2 cha taarifa hii), mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Singida, Dodoma, Njombe, Iringa, Mbeya, Songwe, Rukwa pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro. Hata hivyo, mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi.

Mvua za Msimu zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Oktoba katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Tabora, Katavi, Kigoma, Lindi na Mtwara na kusambaa katika maeneo mengine mwezi Novemba 2026. Mvua hizi zinatarajiwa kuisha kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2027 katika maeneo mengi.

Mvua nyingi zinatarajiwa katika kipindi cha nusu ya kwanza ya msimu (Novemba, 2026 – Januari, 2027), ikilinganishwa na nusu ya pili (Februari – Aprili, 2027). Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa mvua hizo za msimu ni kama ifuatavyo:

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

i. Kanda ya Magharibi (Mikoa ya Tabora, Katavi na Kigoma):

Mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika mikoa hii na zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Oktoba na wiki ya kwanza ya mwezi Novemba, 2026 na kuisha wiki ya nne ya mwezi Aprili na wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2027.

ii. Kanda ya Kati (Mikoa ya Singida na Dodoma):

Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuwa za Juu ya Wastani hadi Wastani na kuanza wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Novemba, 2026 na kuisha wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2027.

iii. Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro):

Mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika maeneo haya. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Novemba, 2026 na kuisha wiki ya nne ya mwezi Aprili na wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2027.

iv. Pwani ya kusini (Mikoa ya Lindi na Mtwara):

Mvua zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Juu ya Wastani katika mikoa hii. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Oktoba na wiki ya kwanza ya mwezi Novemba, 2026 na kuisha wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2027.


v. Maeneo ya kusini mwa nchi (Mkoa wa Ruvuma):

Mvua zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Juu ya Wastani katika mkoa huu. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Desemba, 2026. Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili, 2027.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)



Kielelezo 2: Kushoto: Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2026–Aprili, 2027) na Kulia: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za Msimu (1991–2020).

Angalizo: Mwelekeo wa mvua ulitolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha mvua za Msimu (miezi sita) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi vitazingatiwa katika utabiri wa kila siku na utabiri wa kila mwezi. Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia taarifa za utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi na tahadhari zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

2. MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika kipindi hiki cha Msimu, joto la bahari katika eneo la tropiki ya kati ya Bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuendelea kuwa la Juu ya Wastani, hali inayoashiria mwendelezo wa uwepo wa *El Niño* yenye nguvu kubwa. Aidha, joto la bahari la Juu ya Wastani linatarajiwa zaidi katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi ikilinganishwa na eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi hususan katika kipindi cha nusu ya kwanza ya msimu (Novemba 2026 hadi Januari 2027), hali inayotarajiwa kusababisha upepo wa bahari wenye unyevu kuvuma kuelekea maeneo ya nchi yetu. Vilevile, joto la bahari la Juu kidogo ya Wastani linatarajiwa katika eneo la mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Kwa ujumla, hali hizi za bahari zinatarajiwa kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo mengi ya nchi.

Vilevile, upepo wa magharibi wenye unyevunyevu unatarajiwa kuvuma kutoka misitu ya Kongo kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi na ukanda wa kati na hivyo kuimarisha zaidi mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

3. ATHARI NA USHAURI

Athari za kisekta na ushauri unaotolewa hapa chini umeandaliwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kwa kushirikiana na wataalam wa sekta husika katika mkutano wa wadau wa hali ya hewa uliofanyika tarehe 19 Oktoba, 2026 na semina ya wanahabari iliyofanyika tarehe 21 Oktoba, 2026. Wadau wa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii wanashauriwa kupanga na kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia taarifa mahususi za hali ya hewa zinazotolewa na TMA.

a) Kilimo na Usalama wa Chakula

Vipindi vya unyevunyevu mwingi kupita kiasi kwenye udongo, kutuama kwa maji na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa mazao na kusababisha uharibifu wa miundombinu ya kilimo. Aidha, magonjwa ya mazao yanayosababishwa na fangasi, bakteria na virusi yanatarajiwa kuongezeka. Magonjwa hayo yanaweza kuathiri ukuaji, ubora na mavuno ya mazao mbalimbali, hususan viazi mviringo, alizeti, maharage, ufuta, matunda na mbogamboga. Shughuli za uvunaji, ukaushaji, usafirishaji na uhifadhi wa mazao zinatarajiwa kuathirika kutokana na mvua za muda mrefu na hivyo kuongeza hatari ya upotevu wa mazao baada ya kuvuna. Hata hivyo, shughuli za kawaida za kilimo zinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo wakati wa Msimu huu wa mvua za Msimu 2026/2027.

Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kufanya palizi na kutumia pembejeo sahihi za kilimo kwa wakati. Aidha, wanashauriwa kutumia mbinu na teknolojia bora za kilimo ikiwemo kuanda mifereji, kilimo cha kontua na matuta ili kuzuia kutuama kwa maji mashambani, mmomonyoko wa udongo na upotevu wa rutuba ya udongo. Pia, wanashauriwa kuchagua mbegu na mazao yanayofaa kwa msimu wa mvua za Msimu 2026/2027 na kuendelea kuzingatia ushauri wa maafisa ugani. Vilevile, wanashauriwa kufuatilia kwa karibu taarifa za hali ya hewa zinazotolewa mara kwa mara na Mamlaka ya Hali ya Hewa.

Aidha, wakulima wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya kilimo, kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua, pamoja na kutumia mbinu madhubuti za kudhibiti visumbufu vya mimea na magonjwa ya mazao ili kupunguza upotevu wa mazao na kuongeza tija katika uzalishaji wa kilimo.

b) Mifugo na Uvuvi

Wafugaji na wavuvi wanatarajiwa kunufaika na ongezeko la upatikanaji wa malisho ya mifugo na chakula cha samaki, hivyo kuongeza uzalishaji. Hata hivyo, unyevunyevu mwingi na maji yaliyotumia vinaweza kuongeza hatari ya milipuko ya magonjwa ya mifugo, kama vile homa ya bonde la ufa na kuoza kwa kwato, pamoja na kuongezeka kwa wadudu wanaosambaza magonjwa. Vilevile, kuongezeka kwa maji yanayoingia baharini kunaweza kupunguza kiwango cha chumvi na kuathiri ukuaji na uzalishaji wa mwani, pamoja na kuongeza uwezekano wa magonjwa yanayoathiri mimea ya baharini.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

Wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji, kuhifadhi malisho na kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadaye. Jamii inashauriwa kuweka mipango madhubuti ya matumizi endelevu ya maji na malisho. Wakulima wa mwani wanashauriwa kulima mimea hii kwenye maji ya kina kirefu ili kupunguza au kuzuia athari za maji mengi yanayoingia baharini.

Aidha, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kufuatilia taarifa za hali ya hewa zinazotolewa na Mamlaka, na ushauri kutoka kwa maafisa ugani, na kuchukua hatua stahiki, ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza na kuongeza tija katika msimu huu wa mvua.

c) Utalii na Wanyamapori

Upatikanaji wa malisho na maji kwa wanyamapori katika mbuga na hifadhi za wanyamapori unatarajiwa kuwa mzuri. Hata hivyo, mvua nyingi zinazotarajiwa zinaweza kusababisha kutuama kwa maji na mafuriko, ambayo yanaweza kusababisha wanyamapori kuhama. Hali hii inaweza kusababisha maambukizi ya magonjwa kutoka kwa wanyamapori kwenda kwa wanyama wanaofugwa kutokana na wanyamapori kuingia katika maeneo ya jamii yanayozunguka hifadhi na mapori ya akiba. Hali hiyo inaweza kuongeza uwezekano wa kuongezeka kwa migogoro kati ya binadamu na wanyamapori, na kusababisha hatari kwa binadamu na wanyama wanaofugwa.

Mamlaka husika zinashauriwa kuboresha miundombinu kama vile barabara na mikondo ya kupitisha maji katika hifadhi za wanyamapori na kujenga uelewa kwa jamii ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kutokana na hali ya mvua inayotarajiwa.

d) Usafiri na Usafirishaji

Matukio ya hali mbaya ya hewa yanaweza kuathiri miundombinu na shughuli za usafirishaji ikiwemo njia za barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege. Athari zinazoweza kujitokeza ni pamoja na kuporomoka kwa kingo za barabara, kuchimbika/kuharibika kwa barabara, uharibifu wa madaraja na njia za reli za MGR na SGR hali inayoweza kusababisha kuongezeka kwa ajali na kusimama/ kuchelewa kwa huduma. Aidha, shughuli za upakiaji na upakuaji wa mizigo bandarini zinaweza kuchelewa, hasa kwa shehena zinazohitaji kulindwa dhidi ya unyevu. Pia usafirishaji wa abiria na mizigo kwa kutumia vyombo vya majini vitaathiriwa. Kwa ujumla, hali hizi zinaweza kusababisha kuvurugika kwa huduma za usafirishaji, uharibifu wa mizigo na miundombinu, pamoja na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji na matengenezo.

Kwa upande wa usafiri wa anga, mvua kubwa, radi, upepo mkali vinaweza kusababisha kuathirika kwa shughuli za uendeshaji wa usafiri wa anga ikiwa ni pamoja na kupungua kwa uono, vifaa vya mawasiliano ambavyo vinaweza kusababisha kuchelewa, kubadilishwa kwa ratiba au kusitishwa kwa baadhi ya safari za ndege.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

Wadau wa sekta hii wanashauriwa kuchukua hatua stahiki ikiwemo ukaguzi wa mara kwa mara wa miundombinu ya usafirishaji, na vyombo vya usafiri, na kufanya matengenezo na maboresho stahiki endapo yatahitajika ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

e) Ujenzi

Vipindi vya mvua kubwa vinaweza kuathiri sekta ya ujenzi kwa kuchelewesha miradi na kusababisha migogoro ya kimikataba, kuharibu vifaa na miundombinu, kuongeza gharama za ujenzi, kuathiri ubora wa kazi, na kuhatarisha usalama wa wafanyakazi na watumiaji wa miundombinu mbalimbali hususan katika Barabara, Majengo na Vivuko. Pia, mvua nyingi zinaweza kusababisha mmomonyoko wa udongo, uharibifu wa kazi zilizoanza kutekelezwa na zinazoendelea na utekelezaji kutokana na mafuriko, na kuongezeka kwa unyevu katika maeneo ya ujenzi, hivyo kupunguza uimara wa miundombinu na kusababisha uharibifu wa vifaa kazi au malighafi.

Wadau wanashauriwa kuzingatia utabiri huu wa Msimu katika kuweka sawa mipango ya ujenzi, hasusan katika kipindi kinachotarajiwa kuwa na mvua za Juu ya Wastani. Aidha, wanashauriwa kuchukua hatua stahiki pamoja na kuhamisha mitambo mbalimbali na vifaa vya ujenzi kutoka maeneo ya mabonde na chemchemi kabla ya mvua kuanza ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza. Vilevile inashauriwa kununua mapema vifaa vinavyoweza kuharibika vikipata unyevu, kama saruji na nondo, na kuhifadhi katika maghala salama pamoja na kuweka mifumo thabiti ya usalama mahala pa kazi.

f) Nishati, Maji na Madini

Kuongezeka kwa kina cha maji na uchafuzi katika maziwa, mabwawa, mito na visima kunaweza kujitokeza, hali ambayo inaweza kuathiri vyanzo na miundombinu ya rasilimali za maji, nishati na maeneo ya uchimbaji madini. Aidha, katika maeneo yenye shughuli za uchimbaji mdogo wa madini, tahadhari za usalama zinapaswa kuzingatiwa, kwa kuwa wingi wa mvua unaweza kuongeza hatari ya maporomoko ya ardhi na kuporomoka kwa mashimo ya uchimbaji yasiyo imara.

Wadau wanahimizwa kuendeleza matumizi endelevu na uhifadhi wa rasilimali za maji katika shughuli za uchakataji wa madini, uzalishaji wa umeme, viwanda na matumizi ya majumbani. Ingawa mvua za msimu zinatarajiwa kuongeza upatikanaji wa maji, mamlaka husika zinashauriwa kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji na kuchukua hatua stahiki za kupunguza athari za mafuriko pamoja na kupungua kwa ubora wa maji.

Kwa ujumla, mamlaka husika zinahimizwa kuimarisha ustahimilivu wa vyanzo vya maji na miundombinu ya maji na nishati pamoja na kuendeleza matumizi ya vyanzo mbadala vya nishati ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kutokana na mvua kubwa na mafuriko yanavyoweza kujitokeza.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

g) Mamlaka za Serikali za Mitaa

Vipindi vya mvua kubwa vinaweza kusababisha kutuama kwa maji na mafuriko. Hali hii inaweza kusababisha uharibifu wa miundombinu na upotevu wa maisha na mali. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuboresha mifumo ya mifereji ya maji ili kupunguza athari zinazoweza kusababishwa na mafuriko sambamba na kutoa elimu kwa jamii juu ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha kamati za maafa katika ngazi za vijiji na wilaya ili waweze kujiandaa, kukabiliana na kupunguza athari pindi zitakapotokea.

h) Sekta ya Afya

Magonjwa ya mlipuko yanaweza kujitokeza kutokana na uharibifu wa miundombinu ya maji taka unaoweza kusababishwa na maji kutuama na kutiririka. Mamlaka zinazohusika na afya pamoja na jamii zinashauriwa kuchukua hatua stahiki za kiafya ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza. Hatua hizo ni pamoja na kutokomeza mazalia ya mbu, kuhakikisha upatikanaji wa akiba ya kutosha ya dawa na vifaa tiba, pamoja na kujiandaa kwa changamoto zinazoweza kujitokeza kutokana na uharibifu wa miundombinu ya usafiri. Vituo vya afya vinashauriwa kuwa na mipango mbadala ya kuhakikisha mwendelezo wa huduma za afya.

i) Sekta Binafsi

Sekta binafsi inatarajiwa kunufaika na upatikanaji wa mvua za kutosha katika msimu huu, hususan katika shughuli za kilimo cha kibiashara, uzalishaji viwandani na shughuli nyingine za kiuchumi. Hata hivyo, mvua nyingi kupita kiasi zinaweza kuathiri shughuli za ujenzi wa miundombinu, uzalishaji wa mazao ya kilimo, uhifadhi na usafirishaji wa mazao yanayoharibika haraka, pamoja na bidhaa na mali nyingine

Wadau wa Sekta binafsi wanashauriwa kushirikiana na wataalamu mbalimbali ikiwemo wataalam kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza. Taasisi za Benki na Bima zinashauriwa kuandaa na kutoa huduma mahususi kwa wadau ili kujenga ustahimilivu katika biashara.

j) Menejimenti za Maafa

Vipindi vya mvua kubwa vinatarajiwa kujitokeza na kusababisha mafuriko na maporomoko ya ardhi katika baadhi ya maeneo. Hali hii inaweza kupelekea madhara kwa binadamu, wanyama na mazingira, uharibifu wa miundombinu, kuathiri utoaji wa huduma za kijamii, shughuli za kiuchumi na upotevu wa mali. Hivyo, Idara ya Menejimenti ya Maafa nchini inashauriwa kuendelea kuratibu utekelezaji wa mipango itakayosaidia kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza. Aidha, Sekta, Mamlaka husika, na Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji/Mitaa zinashauriwa kushirikiana na kuchukua hatua stahiki, ikiwa

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

ni pamoja na kutoa tahadhari za mapema, kutoa elimu na miongozo itakayoweza kuzuia au kupunguza madhara, kujiandaa, kukabiliana na maafa, na kurejesha hali endapo maafa yataokea.

k) Vyombo vya Habari

Waandishi wa habari wanashauriwa kutafuta mwongozo wa kitaalamu unaohusu sekta na wataalam husika na kuwasilisha taarifa za hali ya hewa kwa lugha iliyo wazi na rahisi, ili kuongeza uelewa wa umma na kusaidia maandalizi madhubuti dhidi ya athari za hali mbaya ya hewa.

Aidha waandishi wa habari wanashauriwa kupata na kusambaza utabiri na tahadhari rasmi za hali ya hewa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) pekee, ili kuhakikisha taarifa sahihi zinawafikia wananchi kwa wakati kwa ajili ya kuongeza uelewa na kuimarisha maandalizi dhidi ya athari zinazoweza kusababishwa na hali mbaya ya hewa. Kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Na. 2 ya Mwaka 2019, ni kosa kisheria kusambaza taarifa za hali ya hewa kutoka katika vyanzo visivyo rasmi.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wote wa taarifa hii ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, mamlaka za wanyamapori, usafiri na usafirishaji, mamlaka za maji, na afya kuendelea kutafuta, kupata na kuzingatia ushauri wa wataalam katika sekta husika.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa mirejesho ya mwelekeo wa mvua nchini kadiri inavyohitajika. Aidha, wadau wanashauriwa kuwasiliana na Mamlaka ili kupata taarifa mahsusi za utabiri ili kukidhi mahitaji maalum katika sekta zao.

Imetolewa: 23 Oktoba 2026.

Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania:

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)